*Kioo cha Lugha, Juz. 23(1), 16-36*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i1.2

# Mazingira ya Utokeaji wa Alomofu za Utendeshi katika Lugha ya Kimalila

*Azimio Sote*[1]

## Ikisiri

Makala hii inachambua alomofu za utendeshi zinazojitokeza katika vitenzi vya lugha ya Kimalila[2] lengo likiwa kuchambua mazingira ya kutokea kwa alomofu za utendeshi zilizopo na chanzo cha kutokea kwake. Mbinu za uchanganuzi wa matini na hojaji zilitumika kukusanyia data zilizotumika katika utafiti huu. Aidha, Nadharia ya Umboupeo iliongoza utafiti huu. Matokeo yanaonesha kwamba alomofu za utendeshi katika lugha ya Kimalila zipo zinazotokea katika mazingira yanayotabirika na nyingine yasiyotabirika. Lugha ya Kimalila ina alomofu za utendeshi fupi na ndefu. Alomofu fupi ni {-y-}[3] na {-w-} na alomofu ndefu ni {-isy-}, {-izy-}, {-iz-}, {-iziz-}, {-ishiz-}, {-isiz-}, {-wiz-} na {-ikh-}. Alomofu hizi hutokea kutegemeana na kanuni za tangamano la irabu kama ilivyo kwa lugha nyingi za Kibantu. Sifa za mzizi na mfuatano wa utendeshi na utendea zinachochea kwa kiwango kikubwa kutokea kwa alomofu hizi za utendeshi. Mazingira ya kutokea kwa alomofu za utendeshi {-w-}, {-wiz-} na {-iziz-} yanaonesha upekee katika utokeaji wake. Makala inahitimisha kuwa kuna mazingira ya uteuzi na matumizi ya alomofu za utendeshi yanayofungwa na lugha mahususi (Kimalila), jambo linalofungua milango kwa tafiti zaidi katika lugha nyingine kiulinganisho.

## 1.0 Utangulizi

Kwa kawaida mabadiliko ya sauti katika fonolojia yamekuwa yakisababishwa na kuathiriana kwa sauti zinazoandamiana kutoka katika mofu tofauti. Hali hii ina maana kuwa mofolojia ni hitaji la muhimu katika ufafanuzi wa mabadiliko ya sauti

[1] Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mbeya, Tanzania. Baruapepe: azimio.sote@cuom.ac.tz

[2] Kimalila (ɪshɪmalɪla) ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa zaidi katika wilaya ya Mbeya Vijijini, hususani tarafa ya Isangati, katika mkoa wa Mbeya nchini Tanzania. Inabainishwa kwa msimbo wa M24 (Kutsch-Lojenga, 2007).

[3] Alama { } imetumika kumaanisha umbo la kimofolojia (mofu) na kistari – kikimaanisha mpaka wa mofu.

katika kiwango cha kifonolojia. Mabadiliko haya, yanayohusisha viwango vya fonolojia na mofolojia, yanaitwa mabadiliko ya kimofofonolojia (Katamba na Stonham, 2006; Haspelmath na Sims, 2010). Mabadiliko ya kimofofonolojia yanaweza kusababisha mofu kudhihirika katika sura tofauti, matokeo yake ni alomofu kutokea. Wataalamu wamegawanyika katika makundi mawili ya kuielezea dhana ya alomofu. Baadhi ya wataalamu kama vile Mel'cuk, (2006) na Haspelmath na Sims, (2010) wanaeleza kwamba alomofu ni maumbo tofauti yanayowakilisha mofu moja. Katika mtazamo huu, hoja yao inakuwa umbo moja kudhihirika katika sura tofauti zinazoathiriwa na fonolojia. Hata hivyo, wataalamu wengine (Yule, 2006; Katamba na Stonham, 2006; Lieber, 2009 na Cao, 2023) wanafafanua kwamba alomofu ni maumbo kadhaa yanayowakilisha mofimu (maana) moja. Katika mtazamo huu, mofimu inachukuliwa kuwa ni dhana dhahania (maana) inayokuwa akilini ilihali alomofu ni umbo halisi linaloweza kudhihirika kimatamshi na kimaandishi (Cao, 2023). Katika makala hii dhana ya alomofu imetumika kumaanisha maumbo mbalimbali yanayowakilisha mofimu moja. Maumbo haya yanakuwa na umbo la msingi linalotajwa kuwa ni mofu (Haspelmath na Sims, 2010), linalodhihirika katika sura tofauti mazingira yanapobadilika. Kwa mujibu wa Katamba na Stonham (2006), alomofu zinatokea katika mazingira ya kimtoano zikidhihirisha maana moja au dhima ya kisarufi na haziingiliani katika mazingira zinapotokea kwenye neno. Lugha zina tabia ya kufanana na kutofautiana katika baadhi ya vipengele. Makala hii inajikita katika kuchunguza alomofu za utendeshi na utokeaji wake katika lugha ya Kimalila.

Ili kuelewa maandishi ya lugha ya Kimalila, hatuna budi kuelewa kwa ufupi sauti za lugha hii. Lugha ya Kimalila ina jumla ya sauti za konsonanti 23 ambazo ni: vipasuo /p, b, t, d, **j**/[ɟ], **ch**/[ʧ], k, g/; nazali /m, n, **ny**/[ɲ] na **ng'**/[ŋ]; vikwamizi /bh/[**β**], f, v, s, z, **sh**/[ʃ], **kh**/[x] na h/; kimadende /l/, na viyeyusho /**y**/[j] na /w/ (Kutsch-Lojenga, 2007). Katika makala hii, konsonanti zilizowakilishwa kwa umbo moja kimaandishi na kimatamshi zimetumika kama zilivyo. Sauti zilizowasilishwa kwa maumbo mawili ya kimaandishi na kimatamshi, sauti zilizokozwa ndizo zilizotumika katika data za makala hii. Sauti [β] imetumika katika data kwa vile kibadala chake /bh/ hakitumiki katika maandishi ya Kiswahili ilihali sauti nyingine zina vibadala vinavyotumika katika maandishi. Kutsch-Lojenga (2007) anazitaja irabu saba za Kimalila kuwa ni / i,ɩ, a, e, o, ʊ, na u/ ambazo zinaweza kuwa ndefu pia zenye uamilifu wa fonimu na kuzifanya ziwe 14. Irabu zote saba, fupi na ndefu, zimetumika katika data za makala hii.

## 2.0 Mapitio ya Maandiko Mbalimbali

Utendeshi unafafanuliwa kuwa ni namna ya kusababisha au kufanya kitu kiwe tofauti na cha awali, kuwezesha tendo kufanyika, mwigo au msisitizo wa jambo (Schadeberg, 2003). Ikiwa kinyambuo tendeshi kitapachikwa katika kitenzi elekezi, kitasababisha idadi ya yambwa kuongezeka. Aidha, kikipachikwa katika kitenzi sielekezi kitakifanya kitenzi kuwa na uwezo wa kupokea yambwa

(Schadeberg, 2003 na Petzell, 2008). Maumbo ya utendeshi {*-*ɩ*-}[4] na {*-*ɩci*-} yameundwa kama maumbo asilia ya utendeshi katika lugha za Kibantu (Schadeberg, 2003). Hata hivyo, Bostoen na Gu′erois (2022) wanayataja maumbo asilia ya utendeshi ya Kibantu kuwa ni {*-*ɩ*-}, *{*-ɩc-}* na {*-*ɩdi*-}. Wanafafanua zaidi kwamba maumbo haya yametokea katika vipindi tofauti, ambapo maumbo {*-*ɩ*-} *na {*-ɩc-}* yamerithiwa kutoka Niger-Congo ilihali umbo {*-*ɩdi*-} liliundwa katika kipindi cha Mame Bantu.

Maumbo ya vinyambuo vya utendeshi yamekuwa yakibadilika kwa namna tofauti kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa mfano, maumbo {-is-, -ih-, -its- na -is-} yanatumika kubeba dhana ya utendeshi katika lugha za Kishona, Kimakua, Kichewa na Kisoga mtawalia (Hyman na wenzake, 2017) ilihali maumbo {-i, -is, -idz-} yanatumika katika lugha ya Kibena (Morrison, 2011). Hyman (2025) anataja pia umbo (-is-) kuwa linapatikana katika lugha za Ikalanga, Lughanda na Chibemba. Aidha, maumbo ya utendeshi {-i-} na {-ithi} yanatumika katika lugha ya Kikuyu (Waweru, 2011) na Gichucha (Mbaka, 2024) wakati maumbo {-ish-} na {-ik-} yanatumika kuwakilisha dhana ya utendeshi katika lugha ya Kilunda (Kawasha, 2021). Mabadiliko haya yanasababishwa na tofauti za kimofolojia zinazojitokeza katika baadhi ya vipengele kati ya lugha na lugha na hata ndani ya lugha husika kama anavyofafanua Hyman (2003).

Maumbo ya utendeshi yanaweza kubadilika kutokana na sifa za mzizi wa kitenzi au mpangilio wa vinyambuo (Good, 2005; McPheson na Paster, 2009; Morrison, 2011; Hyman na wenzake, 2017) kunakosababisha sauti zinazoandamiana kutoka katika mofu tofauti kuathiriana. Hivyo, baadhi ya sauti katika mzizi au vinyambuo zinalazimika kubadilika, jambo linaloathiri maumbo ya vinyambuo. Kwa mfano, McPherson na Paster (2009) wanaonesha kwamba maumbo ya utendea na utendeshi katika lugha ya Luganda ni {-ir-} na {-is-} mtawalia. Hata hivyo, maumbo haya yanabadilika katika baadhi ya mipangilio ya vinyambuo. Katika utendeshi unapofuatwa na utendea maumbo hayo yanakuwa {-is- + -iz-) ambapo umbo {-ir-} limebadilika kuwa {-iz-}. Aidha, katika mpangilio wa utendea + utendeshi, yanakuwa {-ir- + -iz-} ambapo umbo {-is-} limebadilika kuwa {-iz-}. Mabadiliko ya aina hii yanavifanya vinyambuo kuwa na baadhi ya tabia ambazo ni za pekee ndani ya lugha (Kaoneka, 2009).

Kiango (2008) amebainisha mazingira ya kutokea kwa alomofu {-sh-}, {-z-} na {-y-} katika lugha za Kiswahili. Anafafanua kwamba alomofu {-z-} inatokea katika vitenzi sahili vinavyoishia na irabu pacha ilihali alomofu {-y-} inatokea katika vitenzi ambavyo mizizi inaishia na sauti mojawapo kati ya /z/, /p/ na /w/. Kutokea kwa alomofu hizi kunaongozwa na kanuni za kifonolojia za lugha ya Kiswahili. Ingawa lugha ya Kimalila ni Kibantu, inatofautiana na baadhi ya

[4] * Imetumika kurejelea umbo katika Mame Bantu kwa maana ya Proto Bantu katika Kiingereza (Meeussen, 1967 na Nurse na Watters, 2022). Vilevile, imetumika kumaanisha dhana isiyokubalika.

lugha nyingine za Kibantu. Tofauti hizi zinajitokeza katika baadhi ya kanuni za kifonolojia na pengine hata kimofolojia. Kwa mfano, lugha ya Kimalila hairuhusu mifuatano ya irabu tofauti au pacha (Sote, 2011) zilizotajwa na Kiango (2008).

Uchambuzi wa vinyambua katika vitenzi unakabiliwa na changamoto nyingi. Hyman (2007) anazitaja sababu za changamoto hizo kuwa ni pamoja na uwezo wa vinyambuo kufanana na kutofautiana miongoni mwa makundi ya lugha. Hivyo basi, kunakuwa na ugumu wa kuvielewa na kuvitenga katika vitenzi kwa vile vinahitaji uelewa mpana kuhusu mofolojia ya lugha husika. Pia, vinyambuo vina uwezo wa kutoweka kiurahisi, kuungana, kubadilika na hata kuingiliana kidhima. Kwa mfano, kinyambuo kifupi cha utendeshi {-i-} kimetoweka, na kirefu kina uwezo wa kuungana na kusababisha maboresho ya kimaana katika lugha ya Shiluba (Cocchi, 2008). Mabadiliko haya katika maumbo ya vinyambuo ni ushahidi kwamba alomofu za utendeshi zinaweza kutofautiana katika baadhi ya lugha za Kibantu kama inavyothibitika katika baadhi ya lugha (Good, 2005; Kiango, 2008 na Wesana-Chomi, 2013).

Kutokana na mapitio ya mawazo ya wataalamu mbalimbali hapo juu, ni dhahiri kwamba baadhi ya maumbo ya utendeshi yanakuwa hatarini kupoteza asili yake au kutoweka kabisa kutokana na mabadiliko yanayotokea. Kwa mantiki hii, kila lugha inahitaji kutafitiwa ili kubainisha vinyambuo vya utendeshi na kuvihifadhi kwa ajili ya tafiti nyingine na jamii kwa ujumla. Lugha ya Kimalila bado haijatafitiwa vya kutosha (Kutsch-Lojenga, 2007). Hivyo, makala hii inalenga kuchambua alomofu za utendeshi zinazopatikana katika lugha ya Kimalila pamoja na mazingira yanayosababisha kutokea kwa alomofu hizi.

## 3.0 Nadharia

Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Umboupeo iliyoasisiwa na Prince na Smolensky (1993) na baadaye kufafanuliwa zaidi na McCarthy (2007) na Massamba (2011). Nadharia hii imejengeka katika misingi mitatu ambayo ni zalishi, mashartizuizi na tathmini (Massamba, 2011). Kwanza, zalishi inatekelezwa kwa kuyabaini maumboshindani yanayoelekea kufanana na kuyashindanisha kwa lengo la kupata umbo linalofikia upeo wa kukubalika zaidi kuliko mengine. Massamba (2011) anafafanua zaidi kuwa lugha zina tabia ya kuingiza katika sarufi maumboghafi yasoukomo ambayo yanasababisha maumbotokeo yasoukomo pia. Kwa mantiki hii maumbotokeo haya yanalazimika kushindanishwa ili kupata umbo linaloshinda ambalo linakiuka mashartuzuizi machache zaidi. Pili, kunakuwa na mashartizuizi yanayotumika kupima kukubalika au kutokubalika kwa umbo au muundo husika (Maumbotokeo). Maumbotokeo yanaposhindanishwa yanawezesha kupata umbo, kati ya maumbotokeo, linaloshinda baada ya kuvunja mashartizuizi machache zaidi au kutovunja kabisa. Baadhi ya mashartizuizi katika lugha ya Kimalila ni irabu mbili tofauti hazifuatani, viyeyusho haviwezi kufuatana, na sauti za konsonanti mbili zinaweza kuandamiana kwa sharti la konsonanti ya kwanza kuwa nazali (Sote,

2011). Maumbotokeo katika zalishi yanapimwa kwa kuzingatia mashartizuizi kwa mujibu wa kanuni za lugha husika. Kwa mantiki hii, uchambuzi toshelevu wa data kuhusu sarufi ya lugha husika unapaswa kufanyika kwa lengo la kupata mashartizuizi sahihi. Tathmini ni msingi wa tatu unaotekelezwa kwa kushindanisha maumbotokeo kwa kuzingatia mashartizuizi. Katika hatua hii, maumbo na miundo ya kifonolojia kama vile sauti, silabi na ya kimofolojia kama vile mizizi, shina, neno na viambishi hutathminiwa (Kager, 1999). Hivyo, kipengele cha tathmini ndicho kinachoshindanisha maumbotokeo kwa lengo la kupata umbo linalokubalika au lisilokubalika kutegemeana na kiwango cha mashartizuizi yaliyokiukwa.

Katika makala hii, Nadharia ya Umboupeo ilitumika kushindanisha maumbo ya utendeshi ambayo yalitokana na mabadiliko katika hatua mbalimbali za mageuzi. Umbo lililoelekea kukubalika zaidi kati ya maumbo mawili au zaidi yaliyoshindanishwa ndilo lililochukuliwa kuwa ni sahihi zaidi kuitwa alomofu ya utendeshi. Kwa mfano, maumbo ya utendeshi {-iz-}, {-izi-} na {-izy-} yalishindanishwa kwa lengo la kupata umbo linalokubalika wakati utendeshi unapofuatwa na utendea. Katika muktadha wa matumizi, umbo {-iz-} lilikubalika zaidi kuwa ni la utendeshi pia ikilinganishwa na maumbo {-izi-} na {-izy-}. Vilevile, kuna mazingira ambayo sauti mojawapo katika mzizi wa kitenzi ilibainika kubadilika. Hivyo, mzizi asilia ulishindanishwa na mzizi ulio katika muundo wa nje, katika muktadha wa matumizi ya umbo la utendeshi kwa lengo la kupata mzizi unaokubalika zaidi. Kwa mfano, mazingira ya kutokea kwa umbo la utendeshi {-w-} yanahusiana na mabadiliko ya konsonanti za midomo kuwa vikwamizi vya ufizi; nazali ya midomo ilibainika kuwa haibadiliki ingawa inakubalika.

Kwa mujibu wa Paster (2009), utokeaji wa alomofu za utendeshi unaathiriwa zaidi na mazingira ya kifonolojia. Nadharia ya Umboupeo ina uwezo wa kushughulika na kiwango cha kimofolojia pia kwa kuwa inashughulika na maumbo tofauti ya kimofolojia na ilivyozoeleka kuwa inajikita katika fonolojia tu (Kager, 1999). Kwa mantiki hii, nadharia hii ilifaa zaidi katika makala hii kwa sababu ilikuwa na uwezo wa kutumika katika kutoa ufafanuzi kuhusu mabadiliko ya sauti kwenye maumbo ya utendeshi pamoja na mizizi ya vitenzi. Sauti hizi, kwa kuwa zinakuwa kwenye mofu, zilikuwa na uwezo wa kuelezea mazingira ya utokeaji wa alomofu za utendeshi pia.

## 4.0 Methodolojia

Data za makala hii zilipatikana kwa njia mbili. Zipo zilizokusanywa kutoka Sote (2020) ambapo vitenzi vyenye utendeshi vilikusanywa. Data nyingine zilipatikana kutoka katika *Kamusi ya Kimalila-Kiswahili* (Mwangwale, 2018). Data hizi zilikusanywa kwa njia ya uchanganuzi wa matini. Kwa mujibu wa Ponera (2019), njia ya uchanganuzi wa matini inafaa kutumika katika ukusanyaji wa data zilizo katika maandishi kama vile vitabu, magazeti, hansadi, majarida, kamusi na

ensaiklopedia. Taarifa zake zinatajwa kuwa ni nyoofu na za wazi. Kwa mantiki hii, kamusi ilichukuliwa kwamba ina vitenzi vingi na vyenye sifa mbalimbali.

Watu watatu waliteuliwa kwa lengo la kujaza hojaji zilizokuwa na vitenzi ambavyo vilikuwa havijanyambulishwa. Watoataarifa hawa, waliopatikana kwa njia ya uteuzi kwa lengo maalumu, walikuwa wazawa na wenye umilisi wa lugha ya Kimalila waliokuwa na elimu ya chuo kikuu, waliosoma lugha ya Kiswahili. Ilichukuliwa kwamba elimu na umilisi wao wa lugha ya Kimalila utawapa uwanja mpana katika kuambisha vinyambuo katika vitenzi. Kwa mujibu wa Vaux na Cooper (2003), watoataarifa wachache katika utafiti wa kiisimu wana uwezo wa kutoa taarifa za kutosha kutumika katika kufikia majumuisho katika lugha inayotafitiwa. Hivyo, idadi ya watoataarifa watatu ilichukuliwa kwamba inatosha kwa kuzingatia kuwa data nyingine zilipatikana kutoka chanzo kingine.

Vitenzi vilivyokuwa havijanyambulishwa vilikusanywa kutoka katika kamusi na kuwekwa katika hojaji. Kwa kutumia vitenzi walivyopewa katika hojaji, watoataarifa walifanya unyambulishaji katika hatua tatu: Kwanza, waliambisha vinyambuo vya utendeshi peke yake. Pili, kinyambuo cha utendea kiliambishwa kabla na baada ya utendeshi. Tatu, watoataarifa waliambisha kinyambuo cha utendani, kwa wakati wake, kabla na baada ya utendeshi. Lengo lilikuwa kupata majibu ya maswali matatu: Utendeshi unapokuwa peke yake katika kitenzi unakuwa na umbo gani? Utendeshi unapoandamiana na utendea unawakilishwa kwa umbo gani? Kisha, utendeshi unapoandamiana na utendani unawakilishwa kwa umbo gani? Vinyambuo vya utendea na utendani vilitumika kwa lengo maalumu kwa vile vilichukuliwa kwamba ni rahisi kuandamiana na utendeshi.

Baada ya zoezi la kubaini vitenzi mbalimbali vikiwa na maumbo ya utendeshi kukamilika, mtafiti aliyapitia maumbo ya utendeshi katika vitenzi kwa lengo la kubaini mabadiliko yanayojitokeza kiumbo, pamoja na mazingira ya mabadiliko yake kinapokuwa peke yake au kinapofuatana na vinyambuo vingine. Kwa kufanya hivi, iliwezekana kung'amua mazingira ya utokeaji wa maumbo ya utendeshi katika vitenzi ambavyo vimetumika katika makala hii.

## 5.0 Mazingira Yanayosababisha Alomofu za Utendeshi Kutokea

Maumbo asilia ya utendeshi katika lugha za Kibantu yanatajwa na Bostoen na Gu′erois (2022) kuwa ni {*-*ɩ*-}, {*-*ɩc*-}, na {*-*ɩdi*-}. Maumbo haya yana tabia ya kubadilika katika lugha mbalimbali za Kibantu. Sehemu zifuatazo zinachambua alomofu za utendeshi na mazingira yanayosababisha utokeaji wake katika vitenzi vya lugha ya Kimalila:

### 5.1 Alomofu {-y-} Inatokea katika Mazingira ya Mzizi Kuishia na Nazali /n/, Kikwamizi /s/ au /z/

Umbo la utendeshi {-ɩ-} lenye asili ya Kibantu linadhihirika katika muundo wa nje kama {-y-} katika baadhi ya lugha za Kibantu (Bastin, 1986; Schadeberg, 2003;

Bostoen na Guʼerois, 2022). Utokeaji wa umbo {-y-} unasababishwa na uyeyushaji wa umbo asilia {-i-} linapofuatwa na irabu ishilizi {-a}, kama inavyofafanuliwa na Hyman na wenzake (2017). Lugha ya Kimalila, kama ilivyo kwa lugha nyingine za Kibantu, inatumia umbo {-y-} katika kubeba dhana ya utendeshi badala ya umbo {-i-}. Mazingira ya utokeaji wake katika Kimalila ni ya namna mbili: kwanza ni ikiwa mzizi unaishia na nazali /n/ na pili, ikiwa mzizi unaishia na kikwamizi /s/ au /z/. Mifano katika Jedwali la 1 inaonesha mazingira ya kutokea kwa alomofu ya utendeshi {-y-} katika lugha ya Kimalila.

**Jedwali la 1: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-y-}**

| Na. | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *gon-a* | "lala" | *gon-y-a* | "laza" |
| (b) | *βun-a* | "unguruma" | *βun-**y**-a* | "ungurumisha" |
| (c) | *lɪ:nd-a* | "shinda" | *lɪ:nz-**y**-a* | "shindisha" |
| (d) | *lo:ng-a* | "sema" | *lo:nz-**y**-a* | "semesha" |
| (e) | *sa:t-a* | "sambaa" | *sa:s-**y**-a* | "sambaza" |
| (f) | *sekh-a* | "cheka" | *ses-**y**-a* | "chekesha" |
| (g) | *ge:z-a* | "oga" | *ge:z-**y**-a* | "ogesha" |
| (h) | *fis-a* | "ficha" | *fis-**y**-a* | "fanya mtu afiche kitu (kwa lengo la kukihifadhi)" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 9, 19, 24, 25, 48, 49, 100, 102)

Katika mfano wa Jedwali la 1 mizizi inapoishia na nazali /n/ katika umbo msingi la mzizi, inasababisha alomofu ya utendeshi {-y-} kutokea. Hata hivyo, mizizi inapoishia na sauti ambayo siyo nazali inasababisha sauti hiyo (ya mwisho katika mzizi) kulazimika kubadilika kuwa kikwamizi cha ufizi. Hivyo, sauti /d/, /g/ zimekuwa /z/ na /t/ na /kh/ imebadilika kuwa /s/. Mabadiliko kama haya yameripotiwa pia na Kahigi (2024). Hakuna mabadiliko yaliyotokea katika mizizi kwenye maneno *ge:za* "oga" na *fisa* "ficha", kwa vile mizizi inaishia na sauti /z/ na /s/ mtawalia. Hii ina maana kwamba mabadiliko ya sauti yatatokea ikiwa mzizi utaishia na sauti isiyo nazali itakayolazimika kubadilika kuwa kikwamizi /s/ au /z/ kama sauti inayobadilika itakuwa sighuna au ghuna mtawalia.

Hata hivyo, kinyambuo kinapoishia na nazali /n/ na kufuatwa na utendeshi, kinyambuo cha utendeshi kinakuwa {-y -} bila kuhitaji mabadiliko yoyote ya sauti katika mzizi au kinyambuo cha utendani kinachoishia na sauti /n/. Tazama mifano ifuatayo katika Jedwali la 2.

**Jedwali la 2: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-y-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi + Utendea | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *gog-a* | "ua" | *gog-an-**y**-a* | "sababisha watu wauane" |
| (b) | *te:g-a* | "potea" | *tez-an-**y**-a* | "potezana" |

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi + Utendea | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (c) | *sejel-a* | "sogea" | *sejez-an-**y**-a* | "sogezana" |
| (d) | *shɪmbɪl-a* | "kimbia" | *shɪmbɪz-an-**y**-a* | "kimbizana" |

**Chanzo:** Mwangwale (2018: 25, 102, 106, 120)

Mifano inaonesha kwamba umbo la utendeshi {-y-} limetokea baada ya kutanguliwa na kinyambuo cha utendani kinachoishia na nazali /n/. Inawezekana kuwa mazingira haya yanafanana na yaliyojadiliwa katika Jedwali la 1 (a)-(b) ambapo nazali imetangulia kutokea. Hivyo, kinyambuo {-y-} kinakubalika bila kuathiri umbo msingi la mzizi wala kinyambuo cha utendani. Hivyo basi, alomofu ya utendeshi {-y-} inatokea katika mazingira ya kutanguliwa na mzizi au vinyambuo vinapoishia na nazali /n/ au mzizi unapoishia na kikwamizi cha ufizi /s/ au /z/.

### 5.2 Alomofu {-isy-} Inatokea katika Mazingira Yasiyotabirika

Lugha ya Kimalila inatumia umbo {-isy-} ambalo katika muundo wa ndani ni {-isi-}. Umbo hili huwakilisha dhana ya utendeshi likiwa na alomofu {-esy-} inayotokea kutegemeana na kanuni ya tangamano la irabu. Umbo hili ndilo linalochukuliwa kuwa la msingi katika alomofu zote ndefu za utendeshi katika lugha ya Kimalila. Hii inatokana na sababu ya umbo la asili katika lugha za Kibantu kuwa {-ic(i)-} ambalo linachukuliwa kuwa limebadilika kuwa {-isi-} kutoka katika muundo wa ndani. Alomofu {-isy-} inatumika katika mazingira yasiyotabirika kwa kuwa idadi ya vitenzi vinavyoruhusu matumizi ya alomofu hii ni vichace kuweza kufikia hitimisho sahihi. Tazama mifano katika Jedwali la 3 inayoonesha mazingira ya kutokea umbo la utendeshi katika Kimalila.

**Jedwali la 3: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-isy-}**

| Na. | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *gw-a* | "anguka" | *gw-**isy**-a*[5] | "angusha" |
| (b) | *ly-a* | "la" | *l**ɪ-ɪsy**-a* | "lisha" |
| (c) | *lol-a* | "ona" | *lol-**esy**-a* | "onesha" |
| (d) | *many-a* | "jua" | *many-**ɪsy**-a* | "julisha" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 26, 49, 54, 57)

Katika mazingira ya mfuatano wa umbo {-isi-} na kiambishi tamati {-a} yanasababisha sauti /i/ ya mwisho katika kinyambuo {-isi-} kuyeyushwa na kuwa /y/. Uyeyushaji huu unasababisha alomofu ya utendeshi {-isy-} kutokea. Data

[5] Katika makala hii irabu /i/ inawakilisha irabu /ɪ/ na /e/ ingawa sauti zote zimetumika kutegemeana na tangamano la irabu katika data.

zinaonesha kuwa, katika mazingira haya, kuna mizizi yenye silabi moja ya *gwa* "anguka" na *lya* "kula" na silabi mbili kwenye vitenzi *lola* "ona" na *manya* "jua". Hata hivyo, vitenzi vingine ambavyo vina silabi moja au mbili havikuweza kupokea alomofu hii. Umbo {-isy-} ni miongoni mwa alomofu za utendeshi inayotumika katika baadhi ya lugha za Kibantu (Good, 2005 na Lusekelo, 2012).

### 5.3 Alomofu {-izy-} Inatokea katika Mazingira Changamani

Imeelezwa awali kwamba umbo asilia la utendeshi katika Mame Bantu ni {*-*ɪdi*} ambalo linadhihirika kama {*-ɪzy} kwa baadhi ya lugha za Kibantu (angalia Bostoen na Gu′erois, 2022). Utafiti unaonesha kwamba umbo {-izy-} ni alomofu mojawapo ya utendeshi inayotumika katika lugha ya Kimalila. Alomofu hii inatokea peke yake katika mazingira ya vitenzi vyenye sifa mbalimbali. Hii ina maana kwamba hakuna mazingira maalumu yanayotabirika kwa ajili ya kutokea alomofu {-izy-}. Tazama mifano katika Jedwali la 4.

**Jedwali la 4: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-izy-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *lim-a* | "lima" | *lim-**izy**-a* | "limisha" |
| (b) | *p:ap-a* | "zaa" | *pap-**ɪzy**-a* | "zalisha |
| (c) | *many-a* | "fahamu" | *many-ɪzy-a* | "fahamisha" |
| (d) | *lɪ:ng-a* | "jaribu" | *lɪnj-ɪzy-a* | "jaribisha" |
| (e) | *βo:mb-a* | "fanya" | *βomb-**ezy**-a* | "fanyisha" |
| (f) | *pw-a* | "iva" | *pw-ɪzy-a* | "ivisha" |
| (g) | *lekh-a* | "acha" | *lesh-**ezy**-a* | "achisha" |

**Chanzo:** Mwangwale (2018: 8, 47, 48, 57, 93, 99)

Mifano katika Jedwali la 4 ina vitenzi vyenye mizizi yenye sifa mbalimbali. Katika mazingira haya, baadhi ya vitenzi vimepokea alomofu {-izy-} bila kuruhusu mabadiliko ya sauti kutokea katika mzizi kama katika (a)–(g). Aidha, mabadiliko ya sauti yametokea katika vitenzi viwili kwenye maneno *lɪ:nga* "jaribu" na *lekha* "acha" ambapo sauti /g/ imekuwa /j/ na /kh/ imebadilika kuwa /sh/ mtawalia. Hii ina maana kwamba mazingira ya kutokea alomofu {-izy-} ni zalishi zaidi kwa vile ni rahisi kutokea katika vitenzi vyenye sifa changamani.

Mazingira ya alomofu {-izy-} kutokea yanaingiliana na ya alomofu {-isy-} kwa vile vitenzi vingine vyenye mizizi inayofanana vinaruhusu matumizi yake. Angalia mifano katika Jedwali la 5 ambapo maumbo {-isy-} na {-izy-} yametumika katika mazingira yanayofanana kiutoano ingawa maana zinatofautiana.

**Jedwali la 5: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-isy- na –izy-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *many-a* | "jua/fahamu" | many-***ɪ*****sy**-a | "julisha/fahamisha" |
| (b) | *many-a* | "elewa" | *many-**ɪzy**-a* | "elewesha/fundisha" |
| (c) | *gw-a* | "anguka" | *gw-**isy**-a* | "angusha" |
| (d) | *pw-a* | "iva" | *"pw-**ɪzy**-a* | "ivisha" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 9, 26, 57)

Mazingira ya uteuzi wa {-isy-} au {-izy-} katika Jedwali la 5 yanafanana kwa vile mizizi inafanana. Kitenzi *manya "*jua/elewa" kimepokea alomofu tofauti. Hii ina maana kwamba ingawa alomofu {-izy-} na {-isy-} zinatofautiana kiumbo, zinatokea katika mazingira yanayofanana. Matumizi ya alomofu hizi yanatofautiana na nadharia zinazodai kwamba alomofu tofauti hazitokei katika mazingira yanayofanana kimatamshi (Katamba na Stonham (2006). Inawezekana pia kuwa alomofu {-isy-} ipo katika hatua ya kutoweka katika lugha ya Kimalila kutokana na matumizi yake kuwa machache zaidi ikilinganishwa na ya {-izy-}. Uteuzi huu unazidi kuchagiza hoja iliyowahi kuelezwa awali kuwa baadhi ya tabia za kimofolojia zinakuwa na tofauti zinazopatikana ndani ya lugha mahususi (Hyman, 2003 na Kaoneka, 2009).

### 5.4 Alomofu {-iz-} Inatokea katika Mazingira ya Utendeshi Kufuatwa na Utendea na Mzizi Kuishia na Kikwamizi /s/ au /z/

Lugha ya Kimalila inatumia umbo {-iz -} linalodhihirika kama {-ez-} kutegemeana na kanuni ya tangamano la irabu. Umbo hili linatokea katika mazingira ya utendeshi kufuatwa na utendea {-y-}, ambapo sauti ya mwisho katika mzizi inalazimika kubadilika kuwa kikwamizi /z/ inapofuatiwa na alomofu ya utendeshi {-y-}. Katika mazingira haya, sauti /s/ na /z/ hazitokei katika mzizi msingi. Sauti hizi ni matokeo ya sauti zinazotokea mwishoni mwa mzizi msingi kubadilika kuwa ama /s/ au /z/ kutegemeana na aina ya sauti iliyobadilika kama inavyodhihirika katika Jedwali la 6 hapo chini.

**Jedwali la 6: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-iz-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana | Utendeshi+ Utendea | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | *fikh-a* | "fika" | *fis- **y**-a* | "fikisha" | *fis-**iz**-y-a* | "fikishia" |
| (b) | *shɪl-a* | "pita" | *shɪz-**y**-a* | "pitisha" | *shɪz-**ɪz**-y-a* | "pitishia" |
| (c) | *lo:ngol-a-* | "tangulia/ ongoza" | *longoz-**y**-a* | "ongoza" | *longoz-**ez**-y-a* | "ngozea" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 19, 49, 105)

Mifano inaonesha kwamba utendeshi unapokuwa peke yake unawakilishwa kwa alomofu {-y-}; unapofuatiwa na utendea alomofu ya utendeshi inakuwa {-iz-} au {-ez} ilihali alomofu ya utendea inakuwa {-y-}. Inawezekana kuwa umbo {-iz-} linatokana na udondoshaji wa kiyeyusho /y/ katika {-izy-} baada ya viyeyusho viwili kuandamiana. Kiyeyusho kimoja ni cha sauti iliyo katika umbo la utendeshi [-izy-} na kingine ni kiyeyusho cha utendea {-y-} vinavyofanya muundo wa {-izy-y-} kutokea. Mazingira ya viyeyusho viwili kufuatana hayakubaliki katika fonolojia ya lugha za Kimalila. Hivyo, katika mazingira haya kiyeyusho /y/ kilicho katika utendeshi kinadondoshwa na kufanya umbo {-iz-} kutokea. Umbo la utendea {-y-} haliwezi kudondoshwa katika mazingira haya ili kuepuka kupoteza dhana ya utendea. Badala yake, sauti /y/ iliyo katika utendeshi italazimika kudondoshwa na kufanya umbo {-iz-} au {-ez-} kutokea. Hii ina maana kwamba mabadiliko yanatokea ili kujenga mazingira ya alomofu ya utendea {-y-} kukubalika katika kitenzi, kiumbo na kidhana.

Alomofu {-iz-} inatokea pia katika mazingira ya utendeshi kufuatwa na utendani {-any-}. Lugha ya Kimalila inatumia umbo {-any-} kama alomofu mojawapo ya utendani kati ya alomofu za utendani. Alomofu nyingine za utendani katika Kimalila ni {-an-} na {-a:n-} zinazotokea katika mazingira tofauti kimtoano (Sote, 2020). Tazama mifano katika Jedwali la 7 inayoonesha mazingira ya umbo {-iz-} kutokea utendeshi unapofuatiwa na utendani.

**Jedwali la 7: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-iz-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana | Utendeshi+ Utendani | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | *ku:nt-a* | "gonga" | *kunt-**izy**-a* | "gongesha" | *kunt-**iz**-any-a* | "gongeshana" |
| (b) | *lim-a* | "lima" | *lim-**izy**-a* | "limisha" | *lim-**iz**-any-a* | "limishana" |
| (c) | *βo:mb-a* | "fanya" | *βomb-**ezy**-a* | "fanyisha" | *βomb-**ez**-any-a* | "fanyishana" |
| (d) | *kha:s-a* | "kuna" | *kha:s-**ɪzy**-a* | "sababisha kukuna" | *khas-**ɪz**-any-a* | "sababisha kukunana" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 8, 37, 43, 48)

Mifano hapo juu inaonesha kwamba alomofu ya utendeshi {*-izy-*} inapofuatiwa na umbo la utendani {-any-} inabadilika kuwa {*-iz-*} au {*-ez-*} kutegemeana na kanuni ya tangamano la irabu. Katika mazingira haya, inawezekana kuwa mfuatano wa utendeshi + utendani {-izy + any-} haukubaliki kutokana na ugumu katika kuutamka. Hivyo, mfuatano huu unatanzuliwa kwa kudondosha sauti ya kiyeyusho /y/ iliyo katika alomofu ya utendeshi {-izy-}, na kusababisha alomofu {-iz-} kutokea. Ikiwa udondoshaji huu hautatokea katika mazingira haya, umbo {-izy-} litapoteza dhana ya utendeshi. Hii inadhihirika katika Jedwali la 8 ambapo udondoshaji wa sauti /y/ usipotokea unasababisha alomofu ya utendeshi {-izy-} kutokubalika.

**Jedwali la 8: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-iz-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana | Utendeshi+ Utendani | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | *lim-a* | "lima" | *lim-**izy**-a* | "limisha" | **lim-**izy**-any-a* | "limishana" |
| (b) | *lim-a* | "lima" | *lim-**izy**-a* | "limisha" | *lim-**iz**-any-a* | "limishana" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 48)

Mifano katika Jedwali la 8 inaonesha kwamba neno *limizyanya* halikubaliki ilihali *limizanya* "limishana" linakubalika. Huu ni ushahidi kuwa mazingira ya utendeshi kufuatwa na utendani hayaruhusu alomofu ya utendeshi {-izy-} kutumika.

## 5.5 Alomofu {-iziz-} Inatokea katika Mazingira ya Utendeshi Kufuatwa na Utendea {-y-}

Umbo {-iziz-} linalodhihirika pia kama {-ezez} kutokana na kanuni za tangamano la irabu, linatumika kuwakilisha dhana ya utendeshi katika vitenzi vya Kimalila. Umbo hili linatokea katika mazingira ya utendeshi kufuatwa na utendea {-y-} ambapo umbo la utendeshi linakuwa {-iz-}. Hata hivyo, katika mazingira haya, umbo {-iz-} linalazimika kuradidiwa ili kuunda umbo {-iziz-}. Jedwali la 9 linaonesha mazingira ya kutokea umbo la utendeshi {-iziz-}.

**Jedwali la 9: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-iziz -}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | *pu:t-a* | "sali" | *pu:t-**izy**-a* | "salisha" | *put-**iziz**-y-a* | "salishia" |
| (b) | *lag-a* | "aga" | *laj-**ɪzy**-a* | "agiza" | *laj-**ɪzɪz**-y-a* | "agizia" |
| (c) | *i:mb-a* | "imba" | *ɪ:mb-**ɪzy**-a* | "imbisha" | *ɪmb-**ɪzɪz**-y-a* | "imbishia" |
| (d) | *βo:mb-a* | "fanya" | *βo:mb-**ezy**-a* | "fanyisha" | *βomb-**ezez**-y-a* | "fanyishia" |

**Chanzo:** Mwangwale (2018: 8, 30, 45, 99)

Mifano katika Jedwali la 9 inaonesha kwamba mazingira ya utendeshi kuwa peke yake katika kitenzi yanaruhusu matumizi ya alomofu {-izy/ezy-} lakini katika mazingira ya kufuatwa na utendea, inakuwa {-iziz/ezez-}. Hivyo, katika mazingira ya alomofu ya utendeshi {-izy-} kufuatwa na utendea {-y-} yanasababisha matukio mawili kutokea. Mosi, ni udondoshaji wa sauti /y/ iliyo katika alomofu {-izy-} uliojadiliwa awali. Pili, irabu ndefu iliyo katika mzizi wa kitenzi inafupishwa ili kuendana na kanuni za fonolojia ya Kimalila ambapo irabu ndefu inakuwa fupi pindi maumbo ya vinyambuo yanapoongezeka kama inavyofafanuliwa na Kutsch-Lojenga (2007). Ikiwa uradidi hautafanyika katika mfuatano wa utendeshi na utendea, umbo {-iz-} halitakuwa na hadhi ya utendeshi. Jedwali la 10 linadhihirisha mazingira ya umbo {-iz-} kupoteza maana ya utendeshi ikiwa uradidi hautafanyika.

**Jedwali la 10: Athari za Alomofu ya Utendeshi {-iziz-} Kugawanyika**

| Na | Utendeshi | Maana | Utendesi+ Utendea | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *ɪ:mb-**ɪzy**-a* | "imbisha" | **ɪmb-**ɪz**-y-a* | "imbishia?" |
| (b) | *ɪ:mb-**ɪzy**-a* | "imbisha" | **ɪmb-**ɪzy**-a* | "imbishia" |

**Chanzo:** Mwangwale (2018: 30)

Katika Jedwali la 10 mfuatano wa vinyambuo vya utendeshi na utendea {-iz-y-} hauleti maana ya imbishia ingawa unakuwa na maana katika (b) ambapo alomofu {-izy-} imetumika lakini utendeshi umebaki peke yake. Hii inaonesha kwamba udondoshaji ukitokea bila uradidi wa umbo la utendeshi {-iz-}, unasababisha umbo la utendeshi {-izy-} linalokubalika. Hata hivyo, katika muktadha huu, umbo {-izy-} linapoteza umbo la utendea {-y-}, pamoja na dhana yake, baada ya umbo la utendeshi {-iz-} kuungana na umbo {-y-}. Hivyo, umbo la utendeshi {-iz-} linalazimika kuradidiwa ili kupata alomofu {-iziz-} inayohifadhi zaidi dhana ya utendeshi. Matokeo haya yanaelekea kufanana na yaliyowahi kuripotiwa awali katika lugha za Chitumbuka (Chavula, 2016) na Kishona (Wechsler, 2020). Umbo la utendeshi {-isk-} linaradidiwa kuwa {-isk-isk-} katika Chitumbuka na utendeshi {-is-} unajirudia katika Kishona. Hata hivyo, tofauti inajitokeza katika Chitumbuka kwa vile uradidi unatokea utendeshi unapokuwa peke yake ilihali katika Kimalila uradidi unatokea katika mazingira ya utendeshi kufuatwa na utendea. Kwa upande wa Kishona, dhana ya utendeshi inarudiwa (utendeshi + utendeshi) wakati katika Kimalila hairudiwi.

### 5.6 Alomofu {-ishiz-} Inatokea katika Mazingira ya Utendeshi Kufuatiwa na Utendea {-y-}

Alomofu {-ishiz-} inatumika kuwakilisha dhana ya utendeshi katika lugha ya Kimalila kwenye baadhi ya vitenzi. Umbo hili linatokea katika mazingira ya utendeshi kufuatiwa na utendea unaowakilishwa kwa umbo {-y-}. Vilevile, alomofu {-ishiz-} inatokea katika vitenzi vyenye silabi mbili ambapo silabi ya kwanza inakuwa na irabu ndefu inayofupishwa katika mfuatano wa utendeshi na utendea. Jedwali la 11 linaonesha mazingira ya kutokea alomofu {-ishiz-}.

**Jedwali la 11: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-ishiz -}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana | Utendeshi+ Utendea | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | *sa:m-a* | "hama" | *sa:m-**ɪzy**-a* | "hamisha" | *sam-**ɪshɪz**-y-a* | "hamishia" |
| (b) | *je:nd-a* | "tembea" | *je:nz-**y**-a* | "tembeza" | *jenz-**eshez**-y-a* | "tembezea" |
| (c) | *lɪ:ng-a* | "jaribu" | *lɪnj-**ɪzy**-a* | "jaribisha" | *lɪnj-**ɪshɪz**-y-a* | "jaribishia" |
| (d) | *βo:mb-a* | "fanya" | *βomb-**ezy**-a* | "fanyisha" | *βomb-**eshez**-y-a* | "fanyishia" |
| (e) | *ku:nt-a* | "gonga" | *kunt-**izy**-a* | "gongesha" | *kunt-**ishiz**-y-a* | "gongeshea" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 8, 33, 43, 48, 100)

Katika Jedwali la 11, irabu ndefu zimetoweka katika mifuatano ya utendeshi na utendea. Hii inatokana na irabu ndefu kuwa mbali zaidi kutoka mwishoni mwa neno kama anavyodokeza Kutsch-Lojenga (2007). Aidha, maumbo {-ishiz-} au {-eshez-} yametumika yakiwa na maana ya utendeshi, lakini wenye dhana ya msisitizo pia. Hii ni tofauti na alomofu nyingine zinazokuwa na dhana ya utendeshi tu. Umbo {-ishiz-} linatumika katika mazingira ambayo umbo {-iziz-} linaweza kutumika pia. Kwa mfano, katika 11(a) tunaweza kupata kitenzi *samɪzɪzya* ambapo utendeshi hauwi na maana ya msisitizo ndani yake. Hivyo, ina maana kuwa uteuzi wa umbo {-ishiz-} unaongozwa na lengo la mzungumzaji la kutaka kusisitiza jambo. Ikiwa lengo halitakuwa msisitizo, maumbo mengine ya utendeshi yanatumika.

### 5.7 Alomofu {-isiz} Inatokea katika Vitenzi vyenye Mizizi Inayoishia na Sauti /l/

Katika Jedwali la 11 tumeona jinsi alomofu {-ishiz-} inavyotumika katika mpangilio wa utendeshi unapofuatiwa na utendea. Hata hivyo, data zinaonesha kwamba alomofu {-isiz-} inatumika pia katika mazingira yanayofanana na ya utokeaji wa {-ishiz-}, katika mpangilio wa utendeshi kufuatwa na utendea. Tofauti ni kuwa wakati katika Jedwali la 11 mizizi inakuwa na konsonanti kwa ujumla, katika 12 mizizi inakuwa na kitambaza /l/.

**Jedwali la 12: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-isiz-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana | Utendeshi+utendea | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | *khatal-a* | "poa" | *khatal-**ɪzy**-a* | "poza" | *khatal-**ɪsɪz**-y-a* | "pozea" |
| (b) | *lol-a* | "ona" | *lol-**esy**-a* | "onesha" | *lol-**esez**-y-a* | "oneshea" |
| (c) | *ly-a* | "la" | *lɪ-**ɪsy**-a* | "lisha" | ***lɪ-ɪsɪz** -y-a* | "lishia" |

**Chanzo :** Sote (2020: 104-105)

Katika Jedwali la 12 mzizi una konsonanti /l/ mwanzoni badala ya mwishoni kama ilivyo kwa vitenzi vingine. Inawezekana kuwa mzizi wenye silabi moja, unaoundwa na konsonanti /l/ na kuishia na irabu, unapokea umbo la utendeshi {-isiz-} pia. Hivyo tunaweza kujenga hoja kuwa alomofu {-isiz-} inatumika katika mazingira ya vitenzi vyenye mizizi inayoishia na kitambaza /l/ au kitenzi chenye silabi moja yenye konsonanti /l/ inapofuatiwa na irabu /i/ katika muundo wa ndani.

### 5.7 Alomofu {-w-} Inatokea katika Mazingira ya Mizizi Inayoishia na Vikwamizi /v/ au /f/

Kwa mujibu wa Schadeberg (2003), umbo asilia la utendwa {-ʊ-} linajidhihirisha kama {-w-} katika lugha za Kibantu, mfano katika Kiswahili (Kiango, 2008), Kinyakyusa (Lusekelo, 2012) na Kimalila (Sote, 2020) na (Hyman, 2025). Hata hivyo, kwa upande mwingine, inaonesha kwamba umbo hili linatumika kama alomofu mojawapo ya utendeshi katika lugha ya Kimalila. Alomofu ya utendeshi {-w-} inatumika katika mazingira ya vitenzi ambavyo mizizi inaishia na sauti za vikwamizi /f/ na /v/. Katika mazingira haya, vikwamizi vinatokana na sauti za midomo ambazo zinalazimika kubadilika ama kuwa /f/ au /v/ kama katika Jedwali la 13 linaloonesha mazingira ya kutokea alomofu ya utendeshi {-w-}.

**Jedwali la 13: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-w -}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *laβ-a* | "hangaikaa" | *lav-**w**-a* | "hangaisha" |
| (b) | *zeβ-a* | "legea" | *zev-**w**-a* | "legeza" |
| (c) | *yɪ:mb-a* | "hangaika" | *yɪ:mv-**w**-a* | "hangaisha" |
| (d) | *ye:p-a* | "toka" | *ye:f-w-a* | "sababisha kutoka/ ondoa" |
| (e) | *talip-a* | "refuka" | *talif-**w**-a* | "refusha" |
| (f) | *lam-a* | "waka" | *lam-**w**-a* | "washa" |
| (g) | *fum-a* | "toka" | *fum-**w**-a* | "sababisha kutoka/ toa" |

**Chanzo**: Sote (2020:99)

Mifano katika Jedwali la 13 ina vitenzi vinavyoishia na sauti za midomo ghuna /β/, na vipasuo /b/ na /p/ zinazobadilika kuwa vikwamizi vya midomo-meno /v/ na /f/. Katika mazingira haya, sauti ghuna /β/ na /b/ zinabadilika kuwa kikwamizi ghuna /v/, na sauti sighuna /p/ inakuwa kikwamizi sighuna /f/ ilihali sauti ya midomo /m/ haibadiliki. Ikiwa mzizi utaishia na nazali ya midomo /m/, kinyambuo cha utendeshi kinachoruhusiwa kufuata kinakuwa cha umbo {-w-}. Hii ina maana kwamba alomofu ya utendeshi {-i-} iliyo katika muundo wa ndani (imejadiliwa hapo awali) inajidhihirisha kama {-u-} katika mazingira ya mzizi kuishia na nazali /m/. Katika mazingira haya, sauti ya juu mbele /i/ inabadilika kuwa sauti ya juu nyuma /u/. Hata hivyo, kutokea kwa umbo hili hakuna budi kuchukuliwa kwa tahadhari kwa sababu katika baadhi ya mazingira, kama haya, vitenzi vinapoteza maana. Angalia mifano katika Jedwali la 14.

**Jedwali la 14: Vitenzi Visivyoruhusu Alomofu ya Utendeshi {-w-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *saβ-a* | "ogelea" | **sav-w-a* | "………" |
| (b) | *ji:mb-a* | "jikaza" | **ji:mv-w-a* | "………" |
| (c) | *lem-a* | "shika" | **lem-w-a* | "shikwa" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 33, 47, 100,)

Mifano katika Jedwali la 14 ina vitenzi *savwa*, *ji:mvwa* na *lemwa* ambavyo vinapoteza maana ya utendeshi katika lugha ya Kimalila baada ya kupokea umbo la utendeshi {-w-}. Hii inadhihirisha kwamba kuna mazingira ambapo umbo {-w-} linaweza kubeba dhana ya utendeshi, utendwa, na wakati mwingine linazalisha neno lisilokuwa na maana yoyote pindi linapotumika.

Kwa upande mwingine, tofauti na ilivyojadiliwa awali kuwa mizizi inayoishia na konsonanti za midomo inaruhusu umbo la utendeshi {-w-} kutumika, inaonesha kuwa mzizi unapoishia na konsoananti /kh/ unaweza kuruhusu umbo la utendeshi {-w-} kutumika pia. Hata hivyo, katika mazingira haya, konsonanti ya kikwamizi cha koromeo /kh/ ikitokea mwishoni mwa mzizi msingi, inabadilikaika kuwa kikwamizi cha midomo-meno /f/ na kuruhusu umbo la utendeshi {-w-} kutokea. Hii inadhihirishwa na data katika Jedwali la 15.

**Jedwali la 15: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-w-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *selukh-a* | "hisi kichefuchefu" | *seluf-**w**-a* | "sababisha mtu ahisi kichefuchefu" |

**Chanzo**: Sote (2020: 100)

Hata hivyo, mfano katika Jedwali la 15 unaonesha kwamba utokeaji wa sauti /kh/ unaoruhusu alomofu ya utendeshi {-w-} kutokea siyo zalishi katika lugha ya Kimalila kwa kuwa hatukufanikiwa kupata vitenzi vingine vyenye sifa ya kuishia na sauti /kh/ katika Jedwali la 15. Hata hivyo, vitenzi vingine vyenye mizizi inayoishia na konsonanti /kh/ vinapoambishwa umbo la utendeshi {-w-} vinapoteza maana kwa kuwa maumbo mengine ya utendeshi yanatumika badala yake. Jedwali la 16 linathihirisha kuwa alomofu ya utendeshi {-w-} haiwezi kutokea katika baadhi ya vitenzi vyenye mizizi inayoishia na sauti /kh/.

**Jedwali la 16: Mazingira Yasiyoruhusu Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-w-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *su:kh-a* | "fuka" | *sʊ:f-**w**-a | "………" |
| (b) | *su:kh-a* | "fuka" | *su:s-**y**-a* | "sababisha moshi" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 115)

Inaonesha kuwa alomofu ya utendeshi {-w-} ikitumika katika mazingira ya sauti /kh/ katika mzizi kubadilika kuwa /f/, inasababisha neno lisilokubalika. Hata hivyo, utendeshi unapowakilishwa na umbo {-y-}, unasababisha neno unde kukubalika katika utendeshi, ambapo sauti /kh/ imebadilika kuwa ya ufizi /s/ badala ya kuwa ya midomo-meno /f/. Mazingira yanayomwongoza mzungumzaji kuteua umbo {-y-} na kulikataa {-w-} katika muktadha huu yanashawishi kuwa hizi ni tofauti za ndani ya lugha. Kauli hii iliwahi kudokezwa pia na Kaoneka

(2009) kuwa kuna baadhi ya mabadiliko yanayotokea katika lugha yanakuwa na upekee ndani ya lugha husika.

### 5.8 Alomofu {-wiz-} Inatokea katika Mazingira ya Utendeshi Kufuatwa ya Utendea Mizizi Unapoishia na Sauti ya Midomo

Umbo {-wiz-} ni alomofu mojawapo inayobeba dhana ya utendeshi katika lugha ya Kimalila likiwa ni maboresho ya umbo la utendeshi {-w-}. Alomofu hii inatumika katika mazingira yanayoruhusu umbo la utendeshi {-w-} kutumika ambapo mzizi unaishia na sauti ya midomo kama ilivyojadiliwa awali. Hata hivyo, tofauti yake na mazingira ya {-w-} kutumika, wakati alomofu {-w-} inatumika utendeshi unapotokea peke yake katika kitenzi, alomofu {-wiz-} inatumika utendeshi unapofuatwa na utendea. Hii ina maana kwamba uteuzi wa alomofu hizi unaongozwa na mpangilio wa vinyambuo katika kitenzi. Mifano katika Jedwali la 17 inathibitisha hoja hii ambapo kuna matumizi ya alomofu (-w-} na {-wiz-}.

**Jedwali la 17: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-wiz-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana | Utendeshi+ Utendea | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | *lam-a* | "waka" | *lam-**w**-a* | "washa" | *lam-**wɪz**-y-a* | "washia" |
| (b) | *zʊβ-a* | "panda" | *zʊv-**w**-a* | "pandisha" | *zʊv-**wɪz**-y-a* | "pandishia" |
| (c) | *zeβ-a* | "legea" | *zev-**w**-a* | "legeza" | *zev-**wez**-y-a* | "legezea" |
| (d) | *βo:mb-a* | "fanya" | *βomv-**w**-a* | "fanyisha" | *βomv-**wez**-y-a* | "fanyishia" |

**Chanzo:** Sote (2020: 101)

Awali katika makala hii ilibainishwa kwamba umbo la utendeshi {-iz-} linatumika katika mazingira ya utendeshi kufuatwa na utendea {-y-}. Vilevile, mazingira ya alomofu {-w-} kutumika yameoneshwa kuwa mizizi inaishia na sauti za midomo. Hata hivyo, katika mazingira ya Jedwali la 17, alomofu {-w-} inalazimika kuungana na alomofu ya utendeshi {-iz-} ili kupata alomofu nyingine ya utendeshi {-wiz-}. Hii ina maana kwamba alomofu {-wiz-} ni mahususi katika mazingira ya vitenzi vyenye mizizi inaiyoshia na sauti za midomo lakini utendeshi unapofuatwa na utendea. Umbo {-wiz-} likitenganishwa kupata maumbo {-w-iz-} linapoteza maana, jambo linalothibitisha kwamba umbo hili ni alomofu mojawapo ya utendeshi inayojitosheleza kiumbo na kimaana katika vitenzi vya lugha ya Kimalila.

### 5.9 Alomofu {-ikh-) Inatokea katika Mazingira ya Mizizi ya Vitenzi Kuishia na Sauti za Midomo /p/, /b/, /m/, /β/ au Ufizi /n/

Kwa mujibu wa Schaderberg (2003) umbo asilia la utendeka katika lugha za Kibantu ni {*-ik-}. Hata hivyo, umbo {-ikh-} linatumika kubeba dhana ya

utendeshi pia likiwa limetokana na umbo la Kibantu {*-ɩdi-} (Bostoen na Gu′erois, 2022). Hii inadhihirika pia katika lugha ya Kimalila ambapo umbo {-ikh-} linatumika kama alomofu mojawapo ya utendeshi katika baadhi ya vitenzi. Alomofu hii inatokea katika mazingira ya vitenzi vyenye mizizi inayoishia na sauti za midomo /p/, /b/, /m/ na ufizi /n/. Katika mazingira haya, sauti za midomo hazibadiliki katika mizizi kama ilivyoshuhudiwa katika mazingira ya kutokea alomofu {-w-} ambapo sauti za midomo katika mzizi zinabadilika kuwa /f/ au /v/. Mifano katika Jedwali la 18 inaonesha mazingira ya kutokea alomofu ya utendeshi {-ikh-}.

**Jedwali la 18: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-ikh-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *gu:nzam-a* | "inama" | *gunzam-**ɩkh**-a* | "inamisha" |
| (b) | *pa:p-a* | "beba" | *pap-**ɩkh**-a* | "bebesha" |
| (c) | *vumb-a* | "wa katika vumbi" | *vumb-**ikh**-a* | "zamisha katika vumbi (hasa la moto) |
| (d) | *o:loβ-a* | "lowa" | *oloβ-**ekha**-a* | "sababisha kulowa" |

**Chanzo**: Sote: (2020: 103)

Mifano katika Jedwali la 18 inadhihirisha kuwa umbo {-ikh-} lina alomofu {-ekh-} inayotegemea kanuni ya tangamano la irabu. Hata hivyo, inaonesha pia kuwa alomofu ya utendeshi {-ikh-} inatokea katika mazingira ya mzizi msingi kuishia na nazali /n/ au utendeshi kutokea baada ya utendani unaowakilishwa na alomofu ya utendani {-an-} kama katika Jedwali la 19 linaonesha mazingira ya kutokea alomofu ya utendeshi {-ikh-}.

**Jedwali la 19: Mazingira ya Kutokea Alomofu ya Utendeshi {-ikh-}**

| Na | Utenda | Maana | Utendeshi | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (a) | *gon-a* | "lala" | *gon-**ekh**-a* | "laza (hasa shamba)" |
| (b) | *gon-a* | "lala" | *gon-y-a* | "laza (hasa kiumbe/kitu" |

**Chanzo**: Mwangwale (2018: 25)

Katika Jedwali la 19 kitenzi kina mzizi unaoishia na nazali /n/. Aidha, alomofu ya utendeshi {-ekh} imetumika mahususi kwa maana ya sababisha eneo libaki kwa matumizi ya baadaye". Hata hivyo, alomofu ya utendeshi {-y-} inatumika katika mazingira ambayo {-ekh-} inatumika, lakini kwa maana nyingine za kumlaza mtu, mnyama au kitu. Inawezekana kuwa mazingira ya matumizi ya alomofu {-ekh-} baada ya mzizi unaoishia na nazali ni ya kisitiari zaidi jambo linalokiuka mazingira ya kutokea baada ya sauti za midomo. Hizi ni tofauti nyingine zinazojitokeza ndani ya lugha ambazo Hyman (2007) anatahadharisha kwamba zinahitaji umakini mkubwa kuzielewa.

## 6.0 Hitimisho

Katika makala hii alomofu za mofimu ya utendeshi zinazojitokeza katika vitenzi vya lugha ya Kimalila zimejadiliwa. Imeonesha kwamba kuna alomofu zinazotokea katika mazingira yanayotabirika, ingawa baadhi ya alomofu hizi zinatokea katika mazingira yanayofanana. Kwa mfano, alomofu {-isy-} na {-izy-} zinatokea katika mazingira sawa, ingawa watumiaji wanapendelea zaidi kutumia alomofu {-izy}. Sababu za alomofu {-isy-} kutumika mara chache zaidi ikilinganishwa na umbo {-izy-} haziko wazi. Hata hivyo, alomofu {-isy-} huenda inaelekea katika hatua ya kutoweka katika matumizi. Aidha, alomofu nyingine zinatokea katika mazingira yasiyotabirika, hivyo kuwa vigumu kuufuatilia utokeaji wake. Utokeaji wa alomofu hizi unachochewa kwa kiasi kikubwa na mpangilio wa utendeshi kufuatwa na utendea au utendani, pamoja na sifa za mzizi. Mathalani, utokeaji wa umbo {-wiz-} unaathiriwa na sifa za mzizi na mfuatano wa utendeshi na utendea. Mpangilio wa vinyambuo wa utendeshi kufuatwa na utendea hautumiki kama chanzo cha kutokea kwa alomofu kiupweke, bali katika baadhi ya mazingira, mpangilio huu unaboreshwa na michakato ya udondoshaji, uyeyushaji, uradidi au kuambatanisha vinyambuo tofauti. Makala inahitimisha kwamba baadhi ya mazingira ya utokeaji wa alomofu za utendeshi yanafungamana na lugha mahususi, jambo linalovutia tafiti zaidi kufanyika katika lugha nyingine kiupekee au kiulinganisho.

## Marejeleo


Bastin, Y. (1986). "Les Suffixes Causatifs dans lens Langues Bantoues". *Africana Linguistica*. 5: 55-145.

Bostoen, K. na Guérois, R. (2022). "Reconstructing Suffixal Phrasemes in Bantu Verbal Derivation". Katika K. Bostoen, G. Schryver, R. Guérois na S. Pacchiarotti (Wah.), *On reconstructing Proto-Bantu grammar*. Berlin: Language Science Press. Kur. 343–383

Cao, P. (2023). "Distinction and Examples of Morpheme, Morph and Allomorph in English Linguistics Teaching". Katika *Proceedings of the 2nd International Conference on Education: Current Issues and Digital Technologies* (ICECIDT 2022). DO: 10.2991/978-2-494069-02-2_36. Kur. 323-331. Imesomwa tarehe 25.05.2024.

Chavula, J.J. (2016). *Verbal Derivation and Valency in Citumbuka*. LOT: Leiden University.

Cocchi, G. (2008). "Verbal Extensions in Tshiluba". *Lingua*. 1: 75–89.

Good, J. (2005). "Reconstructing Morpheme Order in Bantu: The Case of Causativization and Applicativization". *Diachronica*. 22: 3–57.

Haspelmath, M. na Sims, A.D. (2010). *Understanding Morphology*. (Tol. 2). London: An Hachette UK Company.

Hyman, L.M. (2003). "Suffix Ordering in Bantu: A Morphocentric Approach". Katika G. Booij na J. van Marle (Wah,), *Yearbook of Morphology*. Dordrecht: Kluwer. Kur 245-281

_______ (2007). "Niger-Congo Verb Extensions: Overview and Discussion". Katika *Selected Preceedings of the 37th Annual Conference on African Linguistics*.

_______ (2025) "Bantu Verb Stem Morphotactics Revisted". Katika L. Clemens, V. Gribaniva, na G. Scontras (Wah), *Syntax in Uncharted Territories: Essays in Honor of Maria Polinsky*. Inapatikana katika DOI: 10.7280/S9M32STT. Kur. 305-324. Imesomwa tarehe 06.04.2025.

Hyman, L.M.; Inkelas, S. na Jenga, F. (2017). "Multiple Exponece in Lusoga Verb Stem". Katika B. Bowern & R. Zanuttini (Wah.), *On Looking into Words (and Beyond)*. Berlin: Language Science Press. Kur 171-189.

Kager, R. (1999). *Optimality Theory*. Cambridge: Cambridge University Press.

Kaoneka, S. (2009). Verb Extensions in Shambala: Their Occurrence and Co-occurrence Constraints. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Katamba, F. na Stonham, J. (2006). *Morphology*. New York: Palgrave Macmillan.

Kawasha, B. (2021). "Imbrication Patterns of Lunda". *Studies in African Linguistics*. *50* (1): 60–82.

Kiango. J.G. (2008). "Sarufi ya Vinyambuo Vitenzi vya Kiswahili: Mitazamo Mbalimbali Kuhusu Kanuni za Unyambuaji". Katika N.O. Ogechi, N.I. Shitemi na K.I. Simila (Wah,). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Nairobi: Moi University Press. Kur 45-59.

Lieber, R. (2009). *Introducing Morphology*. Cambridge: Cambridge University Press.

Kutsch-Lojenga, C.K. (2007). "Minimality and morae in Malila (M. 24)". Katika *37th Annual Conference on African Linguistics.* Cascadilla Proceedings Project. Kur 77-87.

Lusekelo, A. (2012). Inflectional and Derivational Morphology in Optimality Theory: Multiple Object-nouns and Co-ocurrence of Verbal Extension in Kinyakyusa. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Botswana.

Massamba, D.P.B. (2011). *Maendeleo ya Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI

Mbaka, N.K. (2024). "Semantics of -i-, -ith- Causative Morphemes in Gichuka". *Scientia. Technology, Science and Society*. 1(3):145-160. Inapatikana katika DOI: 10.59324/stss. Imesomwa tarehe 06.04.2025.

McCarthy, J.J. (2007). What is Optimality Theory? *Language and Linguistics Compass*. 1(4): 260–291.

McPherson, L. na Paster, M. (2009). "Evidence for the Mirror Principle and Morphological Templates in Luganda Affix Ordering". *Selected Proceedings of the 39th Annual Conference on African Linguistics*", (Wah). A. Ojo and L. Moshi, Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. Kur. 56-66.

Meeussen, A.E. (1967). "Bantu Grammatical Reconstructions". *Africana Linguistica*. 3: 79–120.

Mel'Cuk, I. (2006). *Trends in Linguistics: Aspects of the Theory of Morphology*. Berlin: Mouton W de G Gruyter.

Morrison, E.M. (2011). A Reference Grammar of Bena. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Rice.

Mwangwale, A.T. (2018). *Kamusi ya Kimalila-Kiswahili*. Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.

Nurse. D. na Watters, J.R. (2022). Tense in Proto-Bantu. Katika K. Bostoen, G. Gilles-Maurice de Schryver, R. R. Guérois na S. Pacchiarotti (Wah.), *On Reconstructing Proto-Bantu Grammar*. Berlin: Language Science Press. Kur. 105–171.

Paster, M. (2009). "Explaining Phonological Conditions on Affixation: Evidence from Suppletive Allomorphy and Affix Ordering. *Word Structure.* 2(1): 18–47.

Petzell, M. (2008). *The Kagulu Language of Tanzania Grammar, Texts and Vocabulary*. Cologne: Ruödiger Koöppe Verlag.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dar es Salaam.

Afroplus Industries Limited

Prince, A. na Smolensky, P. (1993). "Optimality Theory: Constraint Interaction in Generative Grammar", Technical Report 2 of the Rutgers Center for Cognitive Science, Rutgers University.

Schadeberg, T.C. (2003). "Derivation". Katika D. Nurse na G. Philippson (Wah,). *The Bantu Languages*. London: Routledge. Kur 71-89.

Sote, A. (2011). Nativization Process of Kiswahili Borrowed Nouns into Shimalila. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

________ (2020). Uchambuzi wa Mnyambuliko wa Vitenzi katika Lugha ya Kimalila. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Vaux, B. na Cooper, J. (2003). *An Introduction to Linguistic Typology.* Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Waweru, M.M. (2011). Gikuyu Verbal Extensions: A Minimalist Analysis. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wechsler, M. (2020). "The Lexical Underspecification of Bantu Causatives and Applicatives". Katika A. Pineda na J. Mateu (Wah,). *Dative Constructions in Romance and Beyond*. Berlin: Language Science Press. Kur. 241-271. Inapatikana katika DOI:10.5281/zenodo.3776551 imesomwa tarehe 06.04.2025.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Yule, G. (2006). *The Study of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.